

DAWA YAKO: Metformin ____ mg

Kwanini ninapatiwa dawa hii? Una kisukari ama uko katika hatari ya kupata kisukari kwani una kiwango kikubwa sana cha sukari kwenye damu yako. Uwepo wa kiwango kikubwa sana cha sukari kwenye damu yako unaweza kusababisha ugonjwa wa moyo, viharusi, ugonjwa wa figo, ama matatizo katika macho yako au mfumo wa neva.

Meza kidonge 1 na chakula kila siku.

Meza kidonge 1 baada ya kupata kifungua kinywa na kidonge 1 baada ya kula mlo wa jioni kila siku.

Meza kidonge 1 baada ya kupata Kifungua Kinywa, kidonge 1 baada ya kula chakula cha mchana na kidonge 1 baada ya kula mlo wa jioni kila siku.

Nitajihisije nitakapokunywa dawa hii? Nyakati nyingine, huwa kuna athari za kimatibabu zinazotokana na kunywa dawa hii. Athari ya kimatibabu ni jambo lile unaloweza kujihisi ambalo si la kawaida. Baadhi ya athari za kimatibabu zinazotokana na kunywa Metformin hutokea pindi mwili wako unapoanza kuizoea dawa hii na zinaweza kujumuisha kichefuchefu, kuharisha, mchafuko wa tumbo, na gesi.

Baadhi ya athari za kitabibu huwa hazitokei mara nyingi, hata hivyo zinaweza kuwa kali sana. **Piga 911 au tembelea Chumba cha Dharura upesi kama utajihisi kupata: mabaka ya ngozi; kuvimba kwa uso, midomo, ulimi ama koo; shida katika kupumua au kukosa pumzi AMA kupata mikazo ya misuli, udhaifu au kuchoshwa sana wakati wa mazoezi makali.**

Nini kingine ninachopaswa kufahamu?

1. Unapaswa kunywa dawa hii kila siku hata pale utakapojihisi kuwa sawa.
2. Unapaswa kuijaza upya dawa hii kila mwezi.
3. Kunywa maji mengi na usikose kupata mlo wowote.
4. Unapaswa kumuona daktari kila baada ya miezi 3 ili kupima kiwango cha sukari kwenye damu yako.
5. Kama utatembelea ofisi ya daktari tofauti, kliniki tofauti ya kitabibu ama chumba tofauti cha dharura, utapaswa kuwataarifu kwamba una shinikizo la juu la damu na kwamba unakunywa dawa ya Metformin.

“Maudhui haya ni ya kwa makusudi ya utoaji taarifa pekee na hayapaswi kuhesabiwa kuwa kama ushauri wa afya wa kitaalamu. Daima tafuta kupata ushauri kutoka kwa Tabibu wako ama mhudumu mwingine wa afya mwenye sifa, kuhusiana na maswali yoyote unayoweza kuwa nayo yanayohusu hali fulani ya kiafya au matibabu.”